CHANJO YA
NDIGANA KALI

Chanja ng'ombe dhidi ya Ndigana kali!
Chanjo moja kwa maisha yote ya ng'ombe!

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.


HILO KUNDI KUBWA LA NDAMA WENYE AFYA NZURI NI LA NANI?
NI NDAMA WA MZEE PARDIRUNI
TENA UKIWAANGALIA VIZURI UTAONA WANA RANGI MASIKIONI
HIZO SIO RANGI, BALI NI HERENI
AMEPATA NDAMA WOTE HAO WAPI NA LINI? MBONA MWAKA JUZI TUU ALIKUWA NA KUNDI DOGO?
HEBU TWENDE TUKAMTEMBELEE ATUELEZE ALIFANYAJE AKAPATA KUNDI KUBWA LA NDAMA WENYE AFYA NZURI NA HERENI MASIKIONI.
ERO SUPAI!
EPA!
SUPAI SHE! UMEPATA WAPI NDAMA WAZURI WENYE HERENI MASIKIONI?
NDAMA WOTE WAMEZALIWA HAPA KWANGU, BALI HAKUNA ALIYEKUFA KWA NDIGANA KALI, NDIYO MAANA WAMEKUWA WENGI.
ULIWEZAJE KUZUIA VIFO KUTOKANA NA HUO UGONJWA HATARI?
NILIWAPATIA CHANJO YA KUZUIA UGONJWA WA NDIGANA KALI MARA TU WALIPOFIKIA UMRI WA MWEZI MMOJA.
HIYO CHANJO NDIYO IKO NDANI YA HIZO HERENI?
HA! HA! HERENI HIZO NI ALAMA YA KWAMBA NDAMA HAO WANA KINGA DHIDI YA UGONJWA HUO HATARI.


KWANI HIYO CHANJO IKOJE? HEBU TUELEZE KWA KIFUPI.
CHANJO NI VIJIDUDU HAI VYA UGONJWA, NA HUDUNGWA CHINI YA SIKIO LA NG'OMBE NA HAPO HAPO NG'OMBE HUCHOMWA SINDANO YA OXY-TETRACYCLINE 30% INAYOFANYA KAZI MWILINI KWA MUDA WA SIKU TANO.
HALAFU, BAADA YA HAPO INAKUWAJE?
MWILI WA NG'OMBE HUPAMBANA NA VIJIDUDU HIVYO NA KUJENGA KINGA. KINGA HII NI YA KUDUMU KATIKA MAISHA YOTE YA NG'OMBE, HOGESHAJI NG'OMBE UNAFANYIKA KWENYE KIPINDI CHA KUPE WENGI TU.
MBONA NI KAMA MUUJIZA?
HAPANA. SIYO MUUJIZA! MMEJIONEA WENYEWE WALE NI NDAMA WA RIKA MBILI TOFAUTI, AMBAO WAMEEPUKA KIFO KUTOKANA NA KUPATIWA CHANJO YA KUZUIA NDIGANA KALI.
JE? NI MTU YEYOTE ANAWEZA KUPATA HIYO HUDUMA YA CHANJO? KWANI GHARAMA YAKE NI KAMA KIASI GANI?
NDIYO, ILI MRADI AWE TAYARI KUFIDIA GHARAMA ZA CHANJO ILI HUDUMA IWE ENDELEVU.
NA SASA TUFANYEJE ILI TUPATE HIYO HUDUMA YA CHANJO YA NDIGANA KALI?
GHARAMA YAKE NI NDOGO SANA UKILINGANISHA NA FAIDA UTAKAYOIPATA. UKITAKA HUDUMA HIYO, WASILIANA NA OFISI YA MIFUGO WILAYANI AU MIKOANI.
AHYA OLE-SERE.

Chanjo ya Ndigana Kali

Chanjo ya Ndigana kali sasa inatengenezwa na Kituo cha Udhibiti wa Kupe na Magonjwa yanayoenezwa na Kupe – *Centre for Ticks and Tick-Borne Diseases* (CTTBD) kilichopo Lilongwe Malawi. Mbeleni, utengenezaji wa chanjo hiyo uliokuwa unafanyika Nairobi, Kenya katika Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo - *International Livestock Research Institute* (ILRI).

Kuhusu Ndigana Kali

Ndigana kali husababisha karibu nusu ya vifo vya ng'ombe wetu. Jibu la tatizo hili ni CHANJO.

Chanjo maana yake ni kuingiza vijidudu hai vya ugonjwa wa Ndigana kali mwilini mwa mnyama kwa lengo la kumpatia kinga dhidi ya shambulio la ugonjwa wenyewe.

Ili chanjo ifanye kazi yake kikamilifu, pia inabidi mnyama adungwe sindano ya Oxytetracycline ambayo husaidia katika kujenga kinga dhidi ya Ndigana kali.

Bei ya Chanjo ya Ndigana Kali

Kwa kawaida, gharama ya chanjo siyo kubwa ukilinganisha na hasara inayotokana na vifo vya mifugo. Mathalani:

- Kifo cha ndama mmoja ambaye thamani yake ni Tshs 80,000 – 90,000 ni sawa na gharama ya kutoa chanjo kwa ndama 6 hadi 8.
- Gharama za chanjo zinazotolewa zinaweza kutofautiana kidogo kati ya mahali na mahali. Tofauti hiyo Zaidi husababishwa na gharama ya usafiri na usafirishaji.

Sifa ya Ng'ombe Anayestahili Kupatiwa Chanjo ya Ndigana Kali

- Ng'ombe mwenye umri wa Zaidi ya mwezi mmoja.
- Ng'ombe asiye na ugonjwa wa aina yeyote.
- Ng'ombe ambaye hajapatiwa chanjo yoyote nyingine katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.
- Ng'ombe ambaye hajapatiwa dawa ya minyoo yenye Levamisole katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Hadi kufikia mwaka 2010 mikoa yote ya Tanzania Bara ilikuwa imepata huduma za Chanjo ya Ndigana kali isipokuwa mkoa wa Ruvuma.

Wafadhili
Global Alliance for Livestock Veterinary Medicines (GALVmed)
(Muungano wa Kimataifa wa Madawa ya mifugo) unaofadhiliwa na Bill & Melinda Gates Foundation pamoja na UK Aid.

Makampuni yanayoweza kuingiza chanjo hiyo nchini toka CTTB Lilongwe, Malawi ni:

Ronheam International
Pamba House, 2nd Floor, Chumba Na. 216
S.L.P 78166 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 0755 327016, 0756 622230

Vetagro Tanzania Ltd
Plot 2A, Corridor Area,
S.L.P 13188, Arusha, Tanzania
Simu: 0786 797071, 027 2544837

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI
Veterinary Complex, 131 Nelson Mandela Road.
S.L.P. 9152, Dar es Salaam.
Simu: 2866446, 2866452

GALVmed
Protecting Livestock – Improving Human Lives